



DAKTARI WA MENO ANAKUJA SHULENI! Pata huduma ya meno shuleni katika BILA GHARAMA* kwako.

* Kwa wagonjwa wanaogharimiwa na Medicaid, Healthwave au Kancare

Jisajili Mtandaoni!
www.MySchoolDentist.com

Skani msimbo
kwa kutumia
simu yako.



Kutunza meno ya mtoto wako ni muhimu ili kuyaweka yakiwa na afya.

RAHISI NA INAYOFAA - Daktari wa meno aliye na leseni ya serikali atachunguza kinywa na meno ya mtoto wako mara kwa mara, pamoja na kutoa huduma ya kusafisha, x-ray inapobidi, matibabu ya floridi na kuweka viziba meno, inavyohitajika. Huduma ya ziada, kama vile kujaza meno, inaweza pia kutolewa. Kadi ya ripoti ya meno itatumwa nyumbani na mtoto wako. Idhini inajumuisha huduma ya awali ya meno na ziara za ufuatiliaji. **TIA SAINI NA URUDISHE SHULENI KWAKO LEO!**

TAFADHALI JAZA

Jina la KWANZA la Kisheria la Mtoto	Jina la MWISHO la Kisheria la Mtoto	Tarehe ya Kuzaliwa mm/dd/yyyy	☐ Kiume ☐ Kike
Anwani	Jiji	Jimbo	Msimbo wa Posta
Shule	Mwalimu		Gredi
Jina la Mzazi/Mlezi	Simu ()		
Barua pepe	Simu Mbadala ()		

SWALI MUHIMU LA AFYA

JE, MTOTO WAKO ANA HALI YOYOTE YA KIAFYA YA ZAMANI AU YA SASA, ULEMAVU, MATATIZO YA TABIA AU MATATIZO MENGINE? TAFADHALI TIA ALAMA KWA KILA HALI INAYOMHUSU MTOTO WAKO NA UELEZE KATIKA NAFASI ILIYOTOLEWA. AMBATANISHA MAELEZO YA ZIADA KWENYE FOMU HII KAMA INAVYOHITAJIKA. KAMA HAKUNA HALI YOYOTE INAYOMHUSU, ACHA WAZI.

- | | | | | |
|---|--|--|---|--|
| ☐ Magonjwa ya kuambukiza | ☐ Mizio - vyakula/msimu | ☐ Matatizo ya kutokwa na damu | ☐ Kisukari | ☐ Ugonjwa wa figo |
| ☐ yanayoendelea (ikiwemo COVID-19) | ☐ Mizio - dawa | ☐ Matatizo ya kupumua | ☐ Matatizo ya moyo | ☐ Ugonjwa wa ini |
| ☐ Pumu | ☐ Matatizo ya tabia | ☐ Matatizo ya meno | ☐ Matatizo ya kinga ya mwili | ☐ Kifafa / Degedege |
| ☐ Mengine _____ | Eleza _____ | | | |

Orodhesha dawa za sasa na/au matatizo ya meno: _____

KAMA MTOTO ANA MEDICAID/HEALTHWAVE/KANCARE

Zungushia duara mojawapo ya vifuatavyo: Healthy Blue, Sunflower, United Healthcare

Ingiza tarakimu 11 za Mtoto
Nambari ya Kitambulisho HAPA: →

--	--	--	--	--	--	--	--	--	--	--

AU # ya Hifadhi ya Jamii ya Mtoto (kama inapataikana)

--	--	--	--	--	--	--	--	--	--	--

BIMA YA MENO YA KIBINAFSI

Bima. Jina la Kampuni (not Medicaid)

Ins. Simu () -

ya Kundi

Jina la Mwajiri

Co. Simu () -

Jina la Mtu Mzima Mwenye Bima

Tarehe ya Kuzaliwa ya Mtu Mzima Mwenye Bima / /

KT cha Mwanachama/ # ya Sera

Mtu Mzima Mwenye Bima SS # - -

IKIWA MTOTO HANA BIMA YA MENO

(TIA ALAMA KWA MOJA HAPA CHINI)

Kama unalipia huduma, ambatisha hundi au hawala ya fedha kwenye fomu hii na uandike ilipwe kwa: **Nevin Waters, DDS**. Ili kulipa kwa kadi ya mkopo, piga simu 855-481-8639.

- ☐ Nitailipia ada iliyopunguzwa kwa ajili ya kusafisha meno, uchunguzi, na floridi kwa kila ziara. Umri wa miaka 12 au mchanga zaidi: **\$57.00** Umri wa miaka 13 au zaidi: **\$70.00**
- ☐ Ninaomba huduma ya msaada ili kulipia gharama za usafishaji wa meno, uchunguzi na floridi kwa mtoto wangu. (Tutakutumia fomu ya maombi ya huduma ya msaada. Inapatikana mara moja tu kwa mwaka wa masomo kwa ajili ya huduma ya kinga pekee.)

Kama mtoto wako anamuona daktari wa meno mara kwa mara, na unataka kuendelea kupata huduma kwa daktari huyo, tafadhali fanya hivyo.

SOMA & USAINI HAPA CHINI

Ninaelewa na kutoa idhini kwa Nevin K. Waters D.D.S., PA (Mtoa Huduma), madaktari wake wa meno washirika au wataalamu wa usafi wa meno, kutoa huduma za meno shuleni kwa mtoto aliyetajwa hapo juu ambaye mimi ni mzazi mwenye haki ya malezi au mlezi halali kisheria, ikiwa ni pamoja na uchunguzi, usafishaji, floridi, viziba meno (sealants), picha za mionzi (x-rays) na upakaji wa Silver Diamine Fluoride kama itakavyohitajika. (Matumizi ya Silver Diamine Fluoride yanaweza kubadili rangi ya matundu yoyote kuwa ya kahawia au nyeusi. TAZAMA NYUMA KWA MAELEZO ZAIDI.) Pia ninatoa idhini ya matibabu mengine yoyote ya meno kama vile kujaza meno, kung'oa meno ya utotoni yenye matatizo, kufanya palpotomi (matibabu ya neva ya jino la utotoni), kuganzisha kinywa na meno, na taratibu nyingine kama itakavyohitajika. Nimesoma SWALI MUHIMU LA AFYA hapo juu na nitaripoti mabadiliko yoyote makubwa katika afya ya mtoto wangu kwa nambari 855-481-8639. Nimesoma ILANI MUHIMU NA IDHINI ILIYO NYUMA YA UKURASA HUU na ninaelewa na kukubaliana na masharti yake.

**SAINI NA ANDIKA
TAREHE HAPA**

Idhini hii inaidhinisha ziara za awali na za baadaye za matibabu ya meno.

TAREHE

**Kwa faragha yako, tafadhali
kunja na ufunge vizuri.**



MASWALI: 855-481-8639 FAKSI: 888-330-4331 Tutembelee katika: BigSmilesDental.org

Nevin K. Waters D.D.S., PA
9393 West 110th Street, Suite 500, Overland Park, KS 66210
© Nevin K. Waters, D.D.S., PA, 2026

4260

KS-COMPR-SWAH-026V1-PDF 00/00

ILANI MUHIMU & IDHINI

Ninaelewa na kutoa idhini kwa Nevin K. Waters, D.D.S., PA (Mtoa Huduma) na madaktari wake wa meno washirika au wataalamu wa usafi wa meno kutoa huduma zifuatazo kwa mtoto aliyetajwa ambaye mimi ni mzazi mwenye haki ya malezi au mlezi halali kisheria: uchunguzi wa meno na maelekezo ya usafi wa kinywa, usafishaji wa meno, matibabu ya floridi, picha za mionzi (x-rays) na viziba meno (sealants), pamoja na upakaji wa Silver Diamine Fluoride ili kutibu kuendelea kwa kuoza kwa meno. Pia ninatoa idhini kwa daktari wa meno kujaza matundu yoyote au kuweka taji kwenye jino, kung'oa meno yoyote ya utotoni yenye matatizo, kufanya palpotomi (matibabu ya neva ya jino la utotoni), kuweka vifaa vya kudumisha nafasi au kufanya matibabu mengine ya meno kama itakavyohitajika. Ninaelewa kwamba kuna hatari katika matibabu ya meno ikiwa ni pamoja na kuvimba au maumivu yanayoweza kutokea kutokana na matibabu au sindano ya dawa ya kuganzisha, au athari za mzio. (Kwa maelezo zaidi kuhusu hatari za matibabu na njia mbadala za matibabu, tafadhali piga nambari iliyotolewa.) Ninaelewa kwamba sehemu ya uchunguzi wa meno wa mtoto wangu inaweza kufanywa kutoka mbali na kwamba taarifa za kitabibu (kama vile picha za mionzi) zinaweza kukusanywa na kutumwa kwa njia ya kielektroniki kwenye kituo kingine kwa ajili ya tathmini ya daktari wa meno. Ninaotoa idhini kwa huduma hizi za matibabu ya meno kwa njia ya mtandao na ninaelewa kwamba, ingawa hatua za kulinda siri zinatumika, matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya wahusika wengine kuseafirisha taarifa yanaweza kuleta hatari za ziada za faragha. Ninaelewa kwamba nina haki ya kupata taarifa za kimatibabu zinazohusiana na huduma za matibabu ya meno kwa njia ya mtandao. Ninatoa idhini na kumwelekeza Mtoa Huduma kutoza na kukusanya malipo kutoka kwa Medicaid, bima, au milipaji mwingine yeyote. Ninatoa idhini kwa shule ya mtoto wangu kutoa taarifa za bima za mtoto wangu kwa Mtoa Huduma na wakala wake wa utozaji ili kumtowa mlipaji kwa huduma. Kama nina bima ya kibinafsi ya meno, nitatozwa na ninakubali kulipa makato yoyote na/au malipo ya kuchangia. Matibabu yanayotolewa na daktari wa meno shuleni yanaweza kuathiri mafao ya baadaye ambayo mtoto wako anaweza kupata chini ya bima ya kibinafsi, Medicaid au CHIP. Isipokuwa kama nimefanya mipango ya awali ya kuhudhuria, na niwepo wakati huduma zinatolewa, huduma zitatolewa bila uwepo wangu. Ninatoa idhini kwa Mtoa Huduma kutuma jumbe fupi za maneno kuhusu mpango wa huduma za meno shuleni. Ninakiri kwamba utumaji wa jumbe fupi za maneno si njia salama ya mawasiliano na unaleta hatari za ziada za faragha. (Gharama za ujumbe na/au data zinaweza kutozwa na mtoa huduma wako wa mawasiliano ya simu; ili kusitisha, jibu "STOP" kwa ujumbe wowote utakaopokea kutoka kwetu. Pia unakubali kupokea simu zilizorekodiwa mapema na/au zinazopigwa kiotomatiki zinazohusiana na mpango wa huduma za meno shuleni kwenye nambari za simu za mezani na/au za mkononi zilizotolewa kwenye fomu hii ya idhini.) Nimepokea Ilani ya Taratibu za Faragha (NPP) iliyoambatishwa kwenye fomu hii na ninatoa idhini ya kutolewa kwa taarifa za rekodi za kimatibabu za mtoto wangu, ikiwa ni pamoja na rekodi zilizopatikana kutoka kwa watoa huduma wengine, na taarifa zozote za VVU/UKIMWI, magonjwa ya kuambukiza, magonjwa ya zinaa, matumizi ya dawa za kulevya na pombe, pamoja na upungufu wa damu. Ninatoa idhini kwa Mtoa Huduma kutoa taarifa hizo kwa mlipaji yeyote anayehusika na/au mtoa huduma za kiutawala na wakandarasi wao wadogo kwa ajili ya matumizi na ufichuzi unaohusiana na matibabu ya mtoto wangu, malipo ya huduma, na madhumuni ya uendeshaji wa huduma za afya. Idhini hii iliyotiwa saini inaidhinisha ziara za awali na za baadaye za mtoto wangu kwa ajili ya matibabu ya meno. Ninaweza kubatilisha idhini hii wakati wowote kwa maandishi.

Silver Diamine Fluoride (SDF) - Matibabu mapya ya meno ya kupambana na matundu ya meno


FAIDA ZA SDF: Matundu ya meno ni ya kawaida kwa watoto, lakini sasa madaktari wetu wa meno wana mbadala salama na usio na maumivu badala ya taratibu za kawaida za kuchimba meno, unaoitwa silver diamine fluoride (SDF). SDF ni dawa ya kiowevu ya antibiotiki iliyoidhinishwa na FDA inayotumika kusaidia kuzuia matundu ya meno yasitokee, yasiuke, au kusambaa kwenye meno mengine. Daktari wa meno hupaka SDF kwa kunusua kwenye meno ya nyuma pekee.

Njia mbadala

- Hakuna matibabu: Jino linaweza kuendelea kuoza na kusababisha maumivu.
- Chaguzi nyingine: rangi ya floridi (fluoride varnish), kuziba jino au taji (filling or crown), au kung'oa jino.

Hatari

- Matibabu ya SDF huenda yasiondoe hitaji la kuziba jino kwa njia ya kawaida.
- Ni kawaida kwa SDF kubadilisha rangi ya tundu la jino kuwa kahawia au nyeusi—hiyo inamaanisha kuwa inafanya kazi.
- Sehemu zenye afya za jino hazitabadiika rangi.
- SDF inaweza kusababisha mabadiliko ya rangi ya muda ikigusana na ngozi. Madoa hayo hayana madhara na yanapaswa kutoweka chini ya wiki moja.
- SDF inaweza kusababisha ladha ya metali ya muda mfupi.



Maswali? Piga simu kwa mmoja wa waratibu wetu wa huduma kwa namba 855-481-8639.

HIFADHI KWA AJILI YA KUMBUKUMBU ZAKO

DR. NEVIN K. WATERS, DDS, P.C.

Sue (Linda) Dobbs, DDS, Staci Osgood, DDS, Nevin Waters, DDS

TAARIFA YA TARATIBU ZA FARAGHA

TAARIFA HII INAFAFANUA JINSI TAARIFA ZA KITABIBU KUHUSU WEWE ZINAVYOWEZA KUTUMIWA NA KUFICHULIWA, NA JINSI UNAVYOWEZA KUPATA IDHINI YA KUFIKIA TAARIFA HIZI. TAFADHALI IHAKIKI KWA UMAKINI. HIFADHI KWA AJILI YA KUMBUKUMBU ZAKO

WAJIBU WETU WA KISHERIA

Faragha ya taarifa zako za kitabibu ni muhimu kwetu. Tunatakiwa na sheria husika za shirikisho na za jimbo kudumisha faragha ya taarifa zako za afya. Tunatakiwa pia kukupa Taarifa hii kuhusu taratibu zetu za faragha, wajibu wetu wa kisheria, na haki zako kuhusiana na taarifa zako za afya. Tunatakiwa kufuata taratibu za faragha zilizozielezwa katika Taarifa hii wakati ambapo inatumika. Tutakuarifu iwapo taarifa zako za kitabibu zisizo salama zimifikwa bila idhini.

Tunahifadhi haki ya kubadilisha taratibu zetu za faragha na masharti ya Taarifa hii wakati wowote, mradi mabadiliko hayo yanaruhusiwa na sheria husika. Tunahifadhi haki ya kufanya mabadiliko katika taratibu zetu za faragha na masharti mapya ya Taarifa yetu kuwa na nguvu kwa taarifa zote za afya tunazozihifadhi, ikiwa ni pamoja na taarifa za afya tulizozielezwa au kuzipokea kabla ya kufanya mabadiliko hayo. Kabla ya kufanya mabadiliko makubwa katika taratibu zetu za faragha, tutabadilisha Taarifa hii na kufanya Taarifa mpya ipatikane ombi litakapowasilishwa.

Unaweza kuomba nakala ya Taarifa yetu wakati wowote. Kwa taarifa zaidi kuhusu taratibu zetu za faragha, au kwa nakala za ziada za Taarifa hii, tafadhali wasiliana nasi kwa kutumia taarifa zilizoorodheshwa mwishoni mwa Taarifa hii.

MATUMIZI NA UFICHUJAJI WA TAARIFA ZA AFYA

Tunatumia na kufichua taarifa za afya kukuhusu kwa madhumuni ya matibabu, malipo, na shughuli za utaji huduma za afya. Kwa mfano:

Matibabu: Tunaweza kutumia au kufichua taarifa zako za afya kwa daktari, muuguzi wa shule/mratibu wa huduma za afya, au mtoa huduma mwingine wa afya anayekupatia matibabu.

Malipo: Tunaweza kutumia na kufichua taarifa zako za afya ili kupata malipo kwa huduma tunazokupatia.

Shughuli za Huduma za Afya: Tunaweza kutumia na kufichua taarifa zako za afya kuhusiana na shughuli zetu za uendeshaji kama vile kukagua uwezo au sifa za wataalamu wa huduma za afya na kutathmini utendaji wa wataalamu na watoa huduma.

Idhini Yako: Matumizi au ufichuzi ambao haujaelezwa vinginevyo katika Ilani hii unaweza kufanywa tu kwa idhini yako ya maandishi. Zaidi ya hayo, lazima tupate idhini yako ya maandishi ili kuwa na kimatibabu au kutumia au kufichua taarifa zako kwa ajili ya kukutangazia bidhaa au huduma ambapo tunalipwa kufanya mawasiliano hayo. Ukikupatia idhini, unaweza kubatilisha kwa maandishi wakati wowote. Kubatilisha kwako hakutaathiri matumizi au ufichuzi wowote ulioruhusiwa na idhini yako wakati lilipokuwa inatumika. Isipokuwa kama utupatia idhini kwa maandishi, hatuwezi kutumia au kufichua taarifa zako za afya kwa sababu yoyote isipokuwa zile zilizozielezwa katika Ilani hii.

Kwa Familia na Marekizi Zako na Watu Wanaohusika katika Utunzaji Wako: Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa mwanafamilia, rafiki au mtu mwingine anayehusika katika utunzaji wako kwa kuwango kinachohitajika ili kusaidia katika huduma yako ya afya au malipo ya huduma yako ya afya. Pia tunaweza kufichua taarifa zako za kimatibabu kwa mashirika ya kutoa msaada ya majanga ili kusaidia kuwatafuta watu wakati wa janga. Pia tunaweza kutumia au kufichua taarifa zako za kimatibabu ili kumjulisha, au kusaidia kumjulisha, mwanafamilia, mgawilishi binafsi au mtu anayehusika na utunzaji wako kuhusu mahali ulipo, hali yako ya jumla au kifo chako. Kama hutaki kufichua taarifa zako za kimatibabu kwa wanafamilia au wengine katika mazingira haya, tafadhali mujulishe Afisa wetu wa HIPAA kwa 888-833-8441.

Inahitajika Kisheria: Tunaweza kutumia au kufichua taarifa zako za afya tunapohitajika kufanya hivyo kisheria.

Usalama wa Umma: Huenda tukahitaji kufichua taarifa za kimatibabu kwa maafisa wa kutekeleza sheria, kama vile kujibu hati ya upekuzi au wito wa mahakama, au kusaidia maafisa wa kutekeleza sheria kumtambua au kumpata mtu, kuripoti vifo ambavyo huenda vimesababishwa na vitendo vya uhalifu, na kuripoti vitendo vya uhalifu katika majengo yetu.

Unyanyasaji au Utekelezaji: Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa mamlaka husika ikiwa tunamini kwa sababu za msingi kwamba huenda wewe ni mwathirika wa unyanyasaji, utekelezaji, au ukatili wa nyumbani au huenda ni mwathirika wa uhalifu mwingine. Tunaweza kufichua taarifa zako za afya kwa kwanza kinachohitajika ili kuzuia tishio kuwa kwa afya au usalama wako au afya au usalama wa wengine.

Vikumbusho vya Miadi: Tunaweza kutumia au kufichua taarifa zako za afya ili kukupa vikumbusho vya miadi (kama vile jumbe za sauti, kadi za posta, barua, barua pepe au jumbe za maandishi).

Shughuli za Usimamizi wa Afya: Tunaweza kufichua taarifa za afya kwa wakala wa usimamizi wa afya kwa shughuli zilizoidhinishwa na sheria. Shughuli hizi za usimamizi zinajumuisha, kwa mfano, ukaguzi wa hesabu, uchunguzi, ukaguzi na tathmini za utaji leseni. Shughuli hizi ni muhimu kwa serikali kufuatilia mfumo wa huduma za afya, milipuko wa magonjwa, mipango ya serikali, uzingatiaji wa sheria za haki za kiraia na kuboresha matokeo ya wagonjwa.

Kesi na Migogoro: Tunaweza kufichua taarifa za afya kukuhusu ili kujibu ombi la mahakama au ya kiutawala. Pia tunaweza kufichua taarifa za afya kukuhusu ili kujibu wito wa mahakama, ombi la ugunduzi au utaratibu mwingine wa kisheria.

Matumizi Mengine na Ufichuzi: Kama inavyoruhusiwa au kuhitajika kisheria, tunaweza kutumia au kufichua taarifa zako za kimatibabu kwa madhumuni ya utafiti; kwa mashirika yanavyoshughulikia na kufuatilia utaji na upandikizaji wa viungo; kwa mipango ya fidia ya wafanyakazi au mipango sawa na hivyo ili kuli sheria zinazohusiana na fidia ya wafanyakazi au mipango sawa inayotoka mafao kwa majaraha au magonjwa yanayohusiana na kazi; kwa shughuli za afya ya umma kama vile kuzuia au kuhidhiti magonjwa, majaraha au ulemavu; kuripoti athari za dawa au matatizo ya bidhaa; kuwajulisha watu kuhusu kuondolewa sokoni kwa bidhaa ambazo huenda wanatumia; kumjulisha mtu ambaye huenda amekaribiana na, au yuko hatarini kuambukizwa au kuneza ugonjwa; kwa wachunguzi wa kimatibabu ili kumtambua mtu aliyefariki au kubaini chanzo cha kifo; au kwa wasimamizi wa mazishi ili kutekeleza majukumu yao.

UFIKIVU WA Haki za Migonjwa: Una haki ya kuangalia au kupata nakala za taarifa zako za afya, isipokuwa katika mazingira machache. Lazima ukawasilie ombi kwa maandishi ili kupata ufikiaji wa taarifa zako za afya na utume ombi lako kwa faksi kwenye nambari iliyowishoni mwa Ilani hii.

Rekodi ya Ufichuzi: Una haki ya kupokea orodha ya baadhi ya ufichuzi ambao sisi au washirika wetu wa kibishara tumefanya kuhusu taarifa zako za afya. Ikiwa utaomba rekodi hii zaidi ya mara moja katika kipindi cha miezi 12, tunaweza kukutoza ada ya kuridhisha inayotegemea gharama, ili kushughulikia maombi haya ya ziada.

Kizuizi: Una haki ya kuomba kwamba tuziele matumizi au ufichuzi wetu wa taarifa zako za afya. Hatulazimiki kukubaliana na ombi lako isipokuwa tu pale ambapo ufichuzi utafanywa kwenye mpango wako wa afya, wewe (au mtu mwingine kwa niaba yako ambaye sio mpango wako wa afya) umelipia kikamilifu huduma yako ya afya, ufichuzi huo unahusiana na malipo au shughuli za huduma za afya, na ufichuzi huo hauhitaji vinginevyo kisheria. Hata hivyo, ikiwa tutakubaliana na kizuizi hicho, tutazingatia makubaliano hayo (isipokuwa katika hali ya dhura).

Mawasiliano Mbadala: Una haki ya kuomba kwa maandishi kwamba tuwasiliane nawe kuhusu taarifa zako za afya kwa njia mbadala au katika maeneo mbadala yaliyobainishwa kwenye ombi lako la maandishi.

Marekebisho: Una haki ya kuomba kwamba turekebisha taarifa zako za afya. Ombi lako lazima liwe la maandishi na lazima lieleze kwa nini taarifa inapaswa kurekebishwa. Tunaweza kukataa ombi lako katika hali fulani.

Ilani ya Kielektroniki: Ikiwa utapokea Ilani hii kwenye tovuti yetu au kwa barua pepe (e-mail), una haki ya kupokea Ilani hii kwa maandishi ukimbia.

MASWALI NA MALALAMIKO

Kama unahitaji maelezo zaidi kuhusu taratibu zetu za faragha au una maswali au wasiwasi, tafadhali wasiliana nasi. Kama una wasiwasi kwamba huenda tumekuka haki zako za faragha, unaweza kuwasilisha malalamiko yako kwetu kwa kutumia maelezo ya mawasiliano yaliyorodheshwa mwishoni mwa Ilani hii. Pia unaweza kuwasilisha malalamiko ya maandishi kwa Ofisi ya Haki za Kiraia ya Idara ya Huduma za Binaadamu ya Marekani kwa kutuma barua kwa 200 Independence Avenue, S.W., Washington, D.C. 20201, kupiga simu kwa 1-877-696-6775, au kutembelea www.hhs.gov/ocr/privacy/hipaa/complaints. Hatutalipiza kisasi kwa njia yoyote ile ukiamua kuwasilisha malalamiko kwetu au kwa Idara ya Afya na Huduma za Binaadamu ya Marekani.

Afisa wa Mawasiliano: Afisa wa HIPAA
Simu: 888-833-8441
Faksi: 888-330-4331
barua pepe: HIPAAOfficer@mobiledentists.com
Tarehe ya Kuanza Kutumika: Novemba 1, 2022